# BARAZA LA MITIHANI LA ZANZIBAR

## TATHMINI YA UFAULU WA WATAHINIWA WALIOFANYA MTIHANI WA KUINGILIA KIDATO CHA TATU MWAKA 2023

## 202 KISWAHILI

Kimetayarishwa na

Baraza la Mitihani la Zanzibar

S. L. P. 3070,

Zanzibar.

©Baraza la Mitihani la Zanzibar, 2024

Haki zote zimehifadhiwa

# YALIYOMO

DIBAJI ........ IV

1.0 UTANGULIZI ........ 1

2.0 SAMPULI YA WATAHINIWA ........ 1

3.1. SEHEMU A: UFAHAMU ........ 1

3.1.1: Swali la 1: Ufahamu ........ 1

3.1.2 Swali la 2: Ufupisho ........ 1

3.2. SEHEMU B: SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA ........ 5

3.2.1 Swali la 3: Sarufi ........ 5

3.2.2 Swali la 4: Sarufi ........ 9

3.2.3 Swali la 5: Matumizi ya Lugha ........ 12

3.3 SEHEMU C: FASIHI SIMULIZI ........ 15

3.3.1 Swali la 6: Fasihi Simulizi ........ 15

3.3.2 Swali la 7: Fasihi simulizi ........ 17

3.3.3 Swali la 8: Fasihi simulizi ........ 20

3.4: SEHEMU D: Uandishi wa Insha na Barua ........ 24

3.4.1 Swali la 9: Uandishi wa Insha ........ 24

3.4.2 Swali la 10: Uandishi wa Barua ........ 29

4.0 HITIMISHO ........ 31

5.0 MAPENDEKEZO ........ 32

VIAMBATANISHO ........ 33

# DIBAJI

Baraza la Mitihani la Zanzibar limeandaa taarifa ya ufaulu wa watahiniwa wa Mtihani wa Kuingilia Kidato cha Tatu katika Somo la Kiswahili Mwaka 2023. Taarifa hii imeandaliwa ili kutoa mrejesho wa ufaulu kwa wanafunzi, walimu, wazazi, waandaaji wa sera, watunga mitaala na jamii kwa ujumla kuhusu ufaulu wa watahiniwa kwa somo hilo.

Mtihani wa Kuingilia Kidato cha Tatu unakusudia kupima kwango cha maarifa waliyoyapata watahiniwa katika miaka miwili ya Sekondari ya Awali. Kupitia matokeo ya Mtihani huu, mtahiniwa hupokea matokeo hayo yanayomuonesha ufaulu kwa lengo la kuweza kuendelea na ngazi nyengine ya elimu au kutoendelea.

Uchambuzi uliowasilishwa katika taarifa hii una lengo la kuelewa kwa undani zaidi sababu za watahiniwa kufanya vizuri au vibaya katika mtihani wao. Taarifa inathibitisha kuwa baadhi ya sababu zilizopelekea watahiniwa wengi kupata alama za juu katika majibu yao ni pamoja na kuelewa matakwa ya swali husika, kuwa na uelewa juu ya dhana mbalimbali zinazohusiana na somo la Kiswahili na kuwa na uwezo wa ubunifu.

Aidha, miongoni mwa sababu zilizobainika na kupelekea baadhi ya watahiniwa kufanya vibaya ni pamoja na kushindwa kufahamu matakwa ya swali husika, kutokuwa na kumbukumbu nzuri kwa yale waliyojifunza, uandishi mbaya na usiofahamika, kukwepa baadhi ya vipengele vya maswali pamoja na kushindwa kutoa majibu sahihi.

Pia, uchambuzi umeonesha vielelezo vya watahiniwa jinsi walivyojibu vizuri au vibaya. Mwisho, uchambuzi huu umetumia machati ambayo yamebainishwa kwa rangi tofauti. Machati hayo yanaonesha ufaulu wa watahiniwa hao kwa kila swali.

Kwa hiyo, Baraza lina imani kuwa mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti hii yatachukuliwa na wadau wa elimu na kuyafanyia kazi kwa lengo la kuinua ufaulu wa somo la Kiswahili katika Mitihani yote inayoandaliwa na Baraza la Mitihani la Zanzibar. Mwisho, Baraza la Mitihani la Zanzibar linatoa shukurani kwa Maafisa wa Mitihani na wote walioshiriki katika kukamilisha Taarifa hii.

**Dkt. RASHID A. MUKKI**



**MKURUGENZI**

**BARAZA LA MITIHANI LA ZANZIBAR**

**ZANZIBAR**

## 1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii inachambua ufaulu wa watahiniwa wa mtihani wa kuingilia Kidato cha Tatu kwa somo la Kiswahili. Mtihani huu ulitungwa kutokana na muhtasari wa Taifa wa mwaka 2010 na muundo wa Mtihani wa Kidato cha Pili wa Baraza la Mitihani la Zanzibar wa mwaka 2015.

Mtihani wa Kiswahili ulikuwa na maswali kumi (10) yaliyogawanyika katika sehemu A, B, C na D. Sehemu A ilikuwa na jumla ya maswali mawili (2) na watahiniwa walitakiwa kujibu maswali yote. Sehemu B ilikuwa na jumla ya maswali matatu (3) na watahiniwa walitakiwa kujibu maswali mawili (2) ambapo swali la tano (5) lilikuwa ni la lazima. Sehemu C ilikuwa na maswali matatu (3) na watahiniwa walitakiwa kujibu maswali mawili (2) ambapo swali la sita (6) ni la lazima na Sehemu D ilikuwa na jumla ya maswali mawili (2) na watahiniwa walitakiwa kujibu swali moja (1).

## 2.0 SAMPULI YA WATAHINIWA

Idadi ya watahiniwa waliofanyiwa Tathmini ni **3,946** sawa na asimia **16.77** ya watahiniwa **23,530** waliosajiliwa kufanya mtihani wa somo hili. Uchambuzi kwa kila swali ulizingatia viwango vitatu vya ufaulu ambavyo ni vibaya, wastani na vizuri ambapo vibaya ulianza alama 0 hadi 29, wastani 30 hadi 64 na vizuri 65 hadi 100. Ufaulu huo umeoneshwa kupitia chati/grafu kwa kutumia rangi tatu ambazo ni: Kijani inawakilisha vizuri, manjano inawakilisha wastani na nyekundu inawakilishavibaya.

## 3.1. SEHEMU A: UFAHAMU

Sehemu hii ilikuwa na jumla ya maswali mawili (2) yaliyotokana na mada ya ufahamu, ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote. Swali la (1) lilikuwa na alama (10) na swali la (2) lilikuwa na alama (10). Hivyo katika sehemu hii kulikuwa na jumla ya alama (20).

### 3.1.1: Swali la 1: Ufahamu

Swali la kwanza lilitokana na mada ya ufahamu ambapo mtahiniwa alitakiwa kuisoma habari aliyopewa na kisha kujibu maswali yaliyotokana na habari hiyo. Swali hili lilikuwa na vipengele vitano (5) kuanzia (i) hadi (v). Kipengele (a) cha swali kilimtaka mtahiniwa kuandika kichwa cha habari kinachofaa kutokana na habari aliyoisoma kwa maneno yasiyozidi matano (5), kipengele (b) kilimtaka mtahiniwa ataje maeneo ambayo mauaji ya vikongwe yanafanyika zaidi nchini Tanzania. Kipengele (c) kilimtaka mtahiniwa ataje sababu inayopelekea vikongwe wengi kuuwawa kikatili. Kipengele (d) kilimtaka mtahiniwa kueleza kwa ufupi namna waganga wa kienyeji wanavyochangia mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi na kipengele (e) kilimtaka mtahiniwa aeleze jambo analoshauri mwandishi lifanyike ili kuzuia mauaji ya kikatili.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima ufahamu na maarifa ya mtahiniwa katika kusoma habari na kujibu maswali kulingana na habari husika.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **3,943** sawa na asilimia **99.92** na watahiniwa **03** sawa na asilimia **0.08** hawakujibu swali hili. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli nambari 1a.

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 2.5 | | 3 - 6 | | 6.5 - 10 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 389 | 9.87 | 1,477 | 37.45 | 2,077 | 52.68 | 3,554 | 90.13 |

**Jadweli nambari 1a: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

Takwimu za Jadweli nambari 1a zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **52.68** upo katika kiwango kizuri ambao umepelekea ufaulu wa jumla kuwa ni mzuri wa asilimia **90.13.**

Aidha, watahiniwa **389** sawa na asilimia **9.87** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na ufahamu wa kuotosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 1.1.

**Kielelezo 1.1 (Kibaya)**

**MASWALI**

a) Andika kichwa cha habari kinachofaa kutokana na habari uliyoisoma kwa maneno yasiyozidi matano (5).

Huyo ni swala la kijiulizo

b) Mauaji ya vikongwe yanafanyika zaidi maeneo gani nchini Tanzania?

Mwanza arusha Vikongwe Tanzania

c) Taja sababu inayopelekea vikongwe wengi kuuwawa kikatili.

Kwa sababu nchi imevaliwa na mabomu na silaha mbali mbali

d) Eleza kwa ufupi namna waganga wa kienyeji wanavyochangia mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi.

pia mnamo miaka iliyopita iliripotiwa kuwa pia kwa mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi yaani albino watu hao matatili huwa chuna ngozi zao au


e) Mwandishi anashauri jambo gani lifanyike ili kuzuia mauaji ya kikatili?

Tatizo hilo linawiyano na yale yanayotokea kando ya ziwa katika eneo hilo wa shiri kina wenye roho kinyama

Kielelezo nambari 1.1 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa ambaye amejibu vibaya swali hili. Mtahiniwa huyu ameshindwa kuifahamu habari aliyoisoma na hivyo kutoa majibu yasiyosahihi kwa maswali yote aliyoulizwa katika swali la kwanza.

Aidha, watahiniwa **2,077** sawa na asilimia **52.68** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hao wanaonekana walikuwa na ufahamu juu ya habari waliyoisoma kama inavyothibitishwa katika kielelezo nambari 1.2

**Kielelezo 1.2 (Kizuri)**


MASWALI

a) Andika kichwa cha habari kinachofaa kutokana na habari uliyoisoma kwa maneno yasiyozidi matano (5).

UHALIFU NA USHIRIKINA TANZANIA.

b) Mauaji ya vikongwe yanafanyika zaidi maeneo gani nchini Tanzania?

Mauaji ya vikongwe yanafanyika zaidi maeneo ya mikoa ya kanda ya ziwa kama vile Shinyanga na Mwanza.

c) Taja sababu inayopelekea vikongwe wengi kuuwawa kikatili.

Sababu inayopelekea vikongwe wengi kuuwawa ni tuhuma za uchawi, wanadaiwa kuuwa ndugu jamaa zao.

d) Eleza kwa ufupi namna waganga wa kienyeji wanavyochangia mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi.

Waganga wa kienyeji wanachangia mauaji ya watu wenye ulemavu kwani wao ndio wanaouziwa hizo ngozi za albino na kuwapatia watu wanaoenda kuwauzia pesa na ngozi hizo hutumika kwa ajili ya ushirikina.

e) Mwandishi anashauri jambo gani lifanyike ili kuzuia mauaji ya kikatili?

Mwandishi anashauri serikali, wananchi na vyombo vya habari kupiga vita unyama huu usikubalike na kuchukuliwa hatua waganga na wateja wao wanaofanya vitendo viovu.

Kielelezo nambari 1.2 ni mfano wa mmoja wa mtahiniwa aliyejibu vizuri swali la kwanza. Mtahiniwa huyo anaonekana kuwa na uelewa wa kutosha juu ya habari aliyoisoma na hivyo katika kipengele (a) amefanikiwa kuandika kichwa cha habari kinachofaa kutokana na habari aliyoisoma kwa maneno yasiyozidi matano (5), katika kipengele (b) ameweza kutaja maeneo ambayo mauaji ya vikongwe yanafanyika zaidi nchini Tanzania, katika kipengele (c) amefanikiwa kuataja sababu inayopelekea vikongwe wengi kuuwawa kikatili, katika kipengele (d) mtahiniwa huyo ameweza kueleza kwa ufupi namna waganga wa kienyeji wanavyochangia mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi na kipengele (e) amaeleza kwa usahihi jambo analoshauri mwandishi lifanyike ili kuzuia mauaji ya kikatili; majibu yaliyopelekea kupata alama za juu katika swali hili.

### 3.1.2 Swali la 2: Ufupisho

Swali hili lilitokana na mada ya ufupisho na lilikuwa na alama 10 ambapo lilimtaka mtahiniwa afupishe kifungu cha habari alichopewa kwa maneno yasiyozidi 20.

Swali hili lililenga kupima kumbukumbu na ujuzi alionao mtahiniwa kuhusu taratibu za ufupisho pamoja na ubunifu katika kufupisha habari mbalimbali.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **3,893** sawa na asilimia **98.66** na watahiniwa **53** sawa na asilimia **1.34** hawakujibu swali hili. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli nambari 1b.

**Jadweli nambari 1b: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 2.5 | | 3 - 6 | | 6.5 - 10 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 664 | 17.06 | 3,115 | 80.02 | 114 | 2.92 | 3,229 | 82.94 |

Takwimu za Jadweli nambari 1b zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **80.02** upo katika kiwango cha wastani ambao umepelekea ufaulu wa jumla kuwa ni mzuri wa asilimia **82.94.**

Aidha, watahiniwa **664** sawa na asilimia **17.06** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na ufahamu wa kutosha juu ya mada ya ufupisho na hivyo kutozingatia kanuni za ufupisho wa habari kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 2.1.

**Kielelezo 2.1 (Kibaya)**


2. Fupisha aya ya mwanzo ya habari uliyoisoma hapo juu kwa maneno yasiyozidi ishirini (20).

habari yangu ni habari ya dereva wa bajaji alikuwa ana endesha bajaji kwa mwendo

Kielelezo nambari 2.1 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa ambaye amejibu vibaya swali hili. Mtahiniwa huyu ameshindwa kabisa kufahamu msingi wa swali hili kwani badala ya kufupisha aya ya mwanzo ya habari aliyoisoma kama swali lilivyomtaka, yeye aliandika habari inayohusu dereva wa bajaji majibu yasiyoendana kabisa na habari aliyopewa.

Aidha, watahiniwa **114** sawa na asilimia **2.92** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa na ufahamu mzuri juu ya mada husika na kuifahamu vyema habari waliyoisoma kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 2.2

**Kielelezo 2.2 (Kizuri)**



2. Fupisha aya ya mwanzo ya habari uliyoisoma hapo juu kwa maneno yasiyozidi ishirini (20).

Imani za kishirikina zimeongezeka nchini Tanzania hali iliyopelekea kuongezeka kwa vitendo vya uhalifu na mauaji ya albino na vikongwe.

Kielelezo nambari 2.2 ni mfano wa mmoja wa mtahiniwa aliyejibu vizuri swali la pili. Mtahiniwa huyu aliweza kufupisha vizuri kifungu cha habari alichopewa huku akizingatia mawazo makuu yaliyomo katika kifungu hicho cha habari, idadi halisi ya maneno na taratibu za ufupisho kama vile matumizi ya lugha yenye kueleweka, kutumia maneno yake mwenyewe pasi na kupotosha habari husika pamoja na matumizi sahihi ya alama na vituo.

### 3.2. SEHEMU B: SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA

Sehemu hii ilikuwa na jumla ya maswali matatu (3) kutoka katika mada ya Sarufi na Matumizi ya lugha. Watahiniwa walitakiwa kujibu maswali mawili (2) ambapo swali la 5 lilikuwa ni la lazima. Kila swali lilikuwa na alama kumi na tano (15) na kuifanya sehemu hii kuwa na jumla ya alama thelathini (30).

#### 3.2.1 Swali la 3: Sarufi

Swali hili lilitokana na mada ya sarufi na liligawika katika vipengele vitano (5) na kila kipengele kilikuwa na vipengele vidogo vidogo ndani yake ambapo kila kipengele kilikuwa na alama tatu (3).

Kipengele (a) cha swali kimtaka mtahiniwa aeleze kazi tatu (3) za viambishi awali kwa kutumia mifano. Kipengele (b) kilimtaka mtahiniwa kutumia mzizi –lim– kuunyumbulisha katika kauli na hali zifuatazo: (i) Urejeshi, (ii) Ukanushi nafsi ya tatu umoja na (iii) Kauli ya kutendea. Kipengele (c) kilimtaka mtahiniwa afafanue kazi za mofimu “ki” kwa kutumia mifano, kazi hizo ni: (i) Kutambulisha udogoshi na (ii) Kutambulisha ushuruti. Kipengele (d) kilimtaka mtahiniwa atumie njia ya uambishaji wa maneno ili kunominisha vitenzi *Nenda* na *Piga* na kipengele (e) kilimtaka mtahiniwa avipange vielezi alivyopewa katika aina zake; vielezi hivyo ni: *vibaya, alfajiri, kiasi kikubwa, humu, mara chache* na *mwaka juzi.*

Kwa ujumla kipengele hiki cha swali kililenga kupima uwezo wa matumizi na kumbukumbu za mtahiniwa kuhusu vipengele mbalimbali vya sarufi kama vile viambishi, mofimu na kazi zake pamoja na aina za maneno.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **2,552** sawa na asilimia **64.67** na watahiniwa **1,394** sawa na asilimia **35.33** hawakujibu swali hili. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli nambari 2a.

**Jadweli nambari 2a: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 4 | | 4.5 – 9.5 | | 10 - 15 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 1,769 | 69.32 | 550 | 21.55 | 233 | 9.13 | 783 | 30.68 |

Takwimu za Jadweli nambari 2a zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **69.32** upo katika kiwango cha vibaya ambao umepelekea ufaulu wa jumla kuwa wa wastani wa asilimia **30.68.**

Aidha, watahiniwa **1,769** sawa na asilimia **69.32** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mada ya vipengele vya sarufi walivyoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 3.1.

**Kielelezo 3.1 (Kibaya)**

3. a) Kwa kutumia mifano eleza kazi tatu (3) za viambishi awali.

i) Viambishi awali hutumika katika kuleta maana ya neno.

ii) Viambishi awali hutumika katika kuunda nomino.

iii) Viambishi awali hutumika katika kuunda sentensi.

b) Tumia mzizi –lim– kuunyumbulisha katika kauli na hali zifuatazo.

i. Urejeshi

Nishalima

ii. Ukanushi nafsi ya tatu umoja

Hulimi

iii. Kauli ya kutendea

Tunalima

c) Kwa kutumia mifano fafanua kazi zifuatazo za mofimu "ki".

i. Kutambulisha udogoshi

Hutumka kuonesha kitu.

ii. Kutambulisha ushuruti

Kutambulisha sababu ya kitu.

d) Kwa kutumia njia ya uambishaji wa maneno, nominisha vitenzi vifuatavyo.

i. Nenda

Nendeni zenu.

ii. Piga

Piga ngoma.

e) Vipange vielezi vifuatavyo katika aina zake.

vibaya, alfajiri, kiasi kikubwa, humu, mara chache, mwaka juzi

Kiasi kikubwa, mara chache, mwaka juzi, alfajiri, humu, vibaya

Kielelezo nambari 3.1 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa ambaye amejibu vibaya swali hili. Mtahiniwa huyu anaonekana kukosa maarifa juu ya mada husika na hivyo kutoa majibu yaliyokwenda kinyume na matakwa ya maswali aliyoulizwa.

Aidha, watahiniwa **233** sawa na asilimia **9.13** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa na ufahamu mzuri juu ya mada husika na kufahamu vyema mantiki ya maswali waliyoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 3.2

**Kielelezo 3.2 (Kizuri)**

3. a) Kwa kutumia mifano eleza kazi tatu (3) za viambishi awali.

i) Viambishi awali hutumika kuonesha wakati au njeo kwa mfano ame-lima wakati uliopita, atakula - wakati ujao
ii) Vile vile viambishi awali hutumika kuonesha nafsi mfano (analima) nafsi ya tatu umoja (wamepigwa) nafsi ya tatu wingi
iii) Pia hutumika kuonesha urejeshi mfano (aliyefika) urejeshi wa kutendea, (anayeandika)

b) Tumia mzizi –lim– kuunyumbulisha katika kauli na hali zifuatazo.

i. Urejeshi
Nina jilimia

ii. Ukanushi nafsi ya tatu umoja
halimi

iii. Kauli ya kutendea
Ana mlimia

c) Kwa kutumia mifano fafanua kazi zifuatazo za mofimu "ki".

i. Kutambulisha udogoshi
Kupachikwa kiambishi "ki" katika neno na kufanya kitu kikawa kidogo mfano kipaka au kimeza

ii. Kutambulisha ushuruti
kuletwa kiambishi ki huweza kuonesha ushurutishi wa jambo fulani katika neno mfano ukilima utapasi, ukila atalia

d) Kwa kutumia njia ya uambishaji wa maneno, nominisha vitenzi vifuatavyo.

i. Nenda
Mwendo

ii. Piga
Pigo

e) Vipange vielezi vifuatavyo katika aina zake.
vibaya, alfajiri, kiasi kikubwa, humu, mara chache, mwaka juzi

Vielezi vya wakati - alfajiri mwaka juzi
Vielezi vya sifa au namna - vibaya
Vielezi vionyeshi aina kuashiria - humu
Vielezi vya idadi - Mara chache na kiasi kikubwa

Kielelezo nambari 3.2 ni mfano wa mmoja wa mtahiniwa aliyejibu vizuri swali la tatu. Mtahiniwa huyo anaonekana kuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya vipengele vya sarufi na hivyo katika kipengele cha 3 (a) amefanikiwa kueleza kazi tatu (3) za viambishi awali kwa kutumia mifano. Kipengele (b) ameweza kutumia mzizi –lim– kuunyumbulisha katika kauli na hali zilizotakiwa. Katika kipengele (c) amefanikiwa kufafanua kwa kutumia mifano kazi za mofimu "ki" katika kutambulisha udogoshi na (ii) Kutambulisha ushuruti.

Aidha, katika kipengele (d) mtahiniwa huyo ameweza kutumia njia ya uambishaji wa maneno ili kunominisha vitenzi *Nenda* na *Piga* na katika kipengele (e) amefanikiwa kuvipanga vielezi alivyopewa katika aina zake kwa usahihi na hivyo kupata alama za juu katika swali hili.

### 3.2.2 Swali la 4: Sarufi

Swali hili lilitokana na mada ya sarufi na liligawika katika vipengele vitano (5) na kila kipengele kilikuwa na vipengele vidogo vidogo ndani yake ambapo kila kipengele kilikuwa na alama tatu (3) na kufanya jumla ya alama zote katika swali hili kuwa ni 15.

Kipengele (a) cha swali kimtaka mtahiniwa ataje aina za maneno yaliyopigiwa mstari katika sentensi "*Wanafunzi waliofika mapema <u>ni</u> mahodari*", "*Kaa hatafuni <u>kwa</u> mdomo*" na "*<u>Ama kweli!</u> Dunia hadaa, ulimwengu ni shujaa*". Kipengele (b) kilimtaka atunge sentensi mbili (2) kwa kutumia viambishi vioneshi kisha aeleze umbali au ukaribu wake na mzungumzaji. Kipengele (c) kilimtaka atafautishe kati ya viwakilishi vya pekee na vivumishi vya pekee. Kipengele (d) kilimtaka aeleze aina mbili (2) za vitenzi vishirikishi vikamilifu kwa kutumia mifano na Kipengele (e) kilimtaka mtahiniwa atumie mifano kutafautisha kati ya vihusishi na vihisishi.

Kwa ujumla kipengele hiki cha swali kililenga kupima kumbukumbu, uundaji na matumizi kupitia vipengele mbalimbali vya sarufi kama vile aina za maneno, sentensi pamoja na kazi za viambishi.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **1,384** sawa na asilimia **35.07** na **2,562** sawa na asilimia **64.92** hawakujibu swali hili. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli nambari 2b.

**Jadweli nambari 2b: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 4 | | 4.5 – 9.5 | | 10 - 15 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 1,290 | 93.21 | 86 | 6.21 | 8 | 0.58 | 94 | 6.79 |

Takwimu za Jadweli nambari 2b zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **93.21** upo katika kiwango cha vibaya ambao umepelekea ufaulu wa jumla kuwa wa vibaya wa asilimia **6.79.**

Aidha, watahiniwa **1,290** sawa na asilimia **93.21** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mada ya vipengele vya sarufi walivyoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 4.1.

**Kielelezo 4. 1 (Kibaya)**

4. a) Taja aina za maneno yaliyopigiwa mstari katika sentensi zifuatazo.

i. Wanafunzi waliofika mapema ni mahodari.

E

ii. Kaa hatafuni kwa mdomo.

V

iii. Ama kweli! Dunia hadaa, ulimwengu ni shujaa.

N

b) Tunga sentensi mbili (2) ukitumia viambishi vioneshi kisha eleza umbali au ukaribu wake na mzungumzaji.

i. Wanafunzi wanasoma darasani leo mzungum zaji huwa wanafunzi wanapenda kuongea namzungumzaji naukaribu wake uko kwenyemaongea

ii. Walimu wanatowa fursa ya kwenda nje yaaninchi mzungumzaji umbali wake na ukaribu wakeuta tumia kwa umbali nisimu kwaukaribu ni lugha.

c) Tafautisha kati ya viwakilishi vya pekee na vivumishi vya pekee.

| Viwakilishi vyapekee | Vivumishi vyapekee |
|---|---|
| Ni aina ya viwakili shi ambavyo huwana maneno maalumu | Ni aina ya vivumishi ambayo huwa kati ka sentensi na maa na |

d) Kwa kutumia mifano eleza aina mbili (2) za vitenzi vishirikishi vikamilifu.

i. Vivumishi

ii. Viunganishi

e) Kwa kutumia mifano tafautisha kati ya vihusishi na vihisishi.

| Vihusishi | Vihisishi |
|---|---|
| Ni aina yamaneno ambayo huonyesha kuso linapofanyika | Ni aina yamaneno ambayo ~~kwa kusisha~~ huhusisha sentensi kuwa kuwa sahihi |

Kielelezo nambari 4.1 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa ambaye amejibu vibaya swali hili. Mtahiniwa huyu anaonekana kukosa msingi juu ya mada husika na hivyo kutoa majibu yaliyokwenda kinyume na matakwa ya maswali aliyoulizwa.

Aidha, watahiniwa **8** sawa na asilimia **0.58** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa na ufahamu mzuri juu ya mada husika na kufahamu vyema mantiki ya maswali waliyoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 4.2

## Kielelezo 4.2 (Kizuri)

4\. a) Taja aina za maneno yaliyopigiwa mstari katika sentensi zifuatazo.

i. Wanafunzi waliofika mapema ni mahodari.

kitenzi kishirikishi (t)

ii. Kaa hatafuni kwa mdomo.

Kihusishi (H)

iii. Ama kweli! Dunia hadaa, ulimwengu ni shujaa.

Kihisishi (I)

b) Tunga sentensi mbili (2) ukitumia viambishi vioneshi kisha eleza umbali au ukaribu wake na mzungumzaji.

i. Juma anasoma kitabu "a" nafsi ya tatu umoja iko mbali na mzungumzaji.

ii. Mimi ninasoma kitabu "ni" nafsi ya kwanza umoja ipo karibu na mzungumzaji.

c) Tafautisha kati ya viwakilishi vya pekee na vivumishi vya pekee.

Viwakilishi vya pekee vinawakilisha nomino inayotajwa kwa kutumia -ote, -enye, -enyewe

Vivumishi vya pekee vinatoa taarifa zaidi kuhusu nomino au kiwakilishi mfano mwenyewe, mwengine

d) Kwa kutumia mifano eleza aina mbili (2) za vitenzi vishirikishi vikamilifu.

i. kitenzi cha mzizi wa -kuwa kinapokaa peke yake katika sentensi mfano Yeye alikuwa hodari.

ii. kitenzi "ni" kinajulisha uyakini wa tendo mfano Paka ni myama mkali.

e) Kwa kutumia mifano tafautisha kati ya vihusishi na vihisishi.

Vihusishi ni maneno yanayoeleza uhusiano wa nomino na mazingira yake mfano amelala juu ya mti.

Vihisishi ni maneno yanayonesha hisia mfano Lo! Ala!, Haya!

Kielelezo nambari 4.2 ni mfano wa mmoja wa mtahiniwa aliyejibu vizuri swali la Nne. Mtahiniwa huyo anaonekana kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu vipengele vya sarufi alivyoulizwa na hivyo katika kipengele cha 3 (a) amefanikiwa kutaja kwa usahihi aina za maneno yaliyopigiwa mstari. Katika kipengele (b) amefanikiwa kutunga sentensi mbili (2) kwa kutumia viambishi vioneshi kisha kueleza umbali au ukaribu wake na mzungumzaji. Katika kipengele (c) ameweza kutafautisha kati ya viwakilishi vya pekee na vivumishi

vya pekee. Katika kipengele (d) amefanikiwa kueleza aina mbili (2) za vitenzi vishirikishi vikamilifu kwa kutumia mifano na Katika kipengele (e) ameweza kutumia mifano kutafautisha kati ya vihusishi na vihisishi; majibu ambayo yamemuwezesha kupata alama za juu katika swali hili.

### 3.2.3 Swali la 5: Matumizi ya Lugha

Swali hili lilitokana na mada ya matumizi ya lugha katika vipengele vya matumizi ya lugha katika miktadha mbalimbali, utata katika tungo, rejista na misimu. Swali hili lilikuwa ni la lazima na liligawanyika katika vipengele vitano (5) "a" mpaka "e". ambapo kila kipengele kilikuwa na alama tatu (3) na kufanya alama zote katika swali hili kuwa ni 15.

Kipengele (a) cha swali hili kilimtaka mtahiniwa aandike mifano ya sentensi zenye makosa ya kisarufi na kimantiki. Kipengele (b) kilimtaka mtahiniwa atoe maana mbili (2) za tungo "*Andika neno vizuri* " na "*Ali kanipigia mpira* ". Kipengele cha (c) kilimtaka mtahiniwa atoe mfano mmoja (1) wa mtindo wa lugha unaotumika katika mazingira ya Shuleni na Mahakamani. Kipengele (d) kilimtaka mtahiniwa kutoa maana za misimu Teja, Utajiju na Buku jero na kipengele (e) kilimtaka mtahiniwa aeleze sifa mbili (2) za lugha ya maandishi.

Kwa ujumla kipengele hiki cha swali kililenga kupima kiwango cha kumbukumbu na maarifa aliyonayo mtahiniwa kuhusu matumizi ya lugha katika miktadha mbalimbali, utata katika tungo, rejista na misimu.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **3,925** sawa na asilimia **99.47** na **21** sawa na asilimia **0.53** hawakujibu swali hili. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli nambari 2c.

**Jadweli nambari 2c: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 4 | | 4.5 – 9.5 | | 10 - 15 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 774 | 19.72 | 1,751 | 44.61 | 1,400 | 35.67 | 3,151 | 80.28 |

Takwimu za Jadweli nambari 2c zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **44.61** upo katika kiwango cha wastani ambao umepelekea ufaulu wa jumla kuwa ni mzuri wa asilimia **80.28.**

Aidha, watahiniwa **774** sawa na asilimia **19.72** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na msingi mzuri kuhusu mada husika kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 5.1

**Kielelezo 1.5 (Kibaya)**

5. a) Andika mifano ya sentensi zenye makosa yafuatayo.

i. Kosa la kisarufi

Kosa la ubakaji .

ii. Kosa la kimantiki

Kosa lo kisheria

b) Toa maana mbili (2) kwa kila tungo zifuatazo.

i. Andika neno vizuri.

huyu mtoto amefauku vizuri
Asha ana soma vizuri
mimi na soma vizuri

ii. Ali kanipigia mpira.

Ali ana nipigia mpira
Ali ana cheza mpira

c) Toa mfano mmoja (1) wa mtindo wa lugha unaotumika katika mazingira yafuatayo.

i. Shuleni

mazingira ya skuli ni mazingira ni mazuri sana

ii. Mahakamani

mazingira ya mahakamani ni mazingira yanayo sababisha marazi

d) Toa maana za misimu ifuatayo.

i. Teja

ii. Utajiju

iii. Buku jero

e) Eleza sifa mbili (2) za lugha ya maandishi.

i. lugha ni sehemu ambayo inotumika kama skuli

ii. lugha ni sehemu ambayo inotumika kama mahakamani

Kielelezo nambari 5.1 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa ambaye amejibu vibaya swali hili. Mtahiniwa huyu ameshindwa kabisa kufahamu msingi wa swali hili na hivyo kutoa majibu yaliyokwenda kinyume na matakwa ya swali husika. Kwa mfano katika kipengele cha 5 (a) mtahihiwa badala ya kuandika sentensi zenye makossa ya kisarufi na kimantiki yeye ametaja aina za makosa. Pia mtahiniwa huyu ameshindwa kabisa kujaribu katika kipengele 5 (d) majibu ambayo yamepelekea kupata alama za chini katika swali hili.

Aidha, watahiniwa **1,400** sawa na asilimia **35.67** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa na ufahamu mzuri juu ya mada husika na kufahamu vyema mantiki ya maswali waliyoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 5.2

**Kielelezo 5.2 (Kizuri)**

5. a) Andika mifano ya sentensi zenye makosa yafuatayo.

i. Kosa la kisarufi

Naumwaga. Badala ya naumwa.

ii. Kosa la kimantiki

Nilikwenda nilimkuta hayupo. Badala ya Nilikwenda hayupo.

b) Toa maana mbili (2) kwa kila tungo zifuatazo.

i. Andika neno vizuri.

i) Andika neno kwa usahihi.
ii) Andika neno linaloitwa "vizuri"

ii. Ali kanipigia mpira.

i) Ali kanipiga kwa kutumia mpira.
ii) Ali kanipiga kwa sababu ya mpira.

c) Toa mfano mmoja (1) wa mtindo wa lugha unaotumika katika mazingira yafuatayo.

i. Shuleni

~~Kesaanyeni~~ ~~Drabuto~~ ya Kusanyeni madaftari ya Kiswahili.

ii. Mahakamani

Shauri kufungua nambari 019/023.

d) Toa maana za misimu ifuatayo.

i. Teja

Mtu ~~ateep~~ anaevuta unga wa bangi.

ii. Utajiju

Pambana na hali yako.

iii. Buku jero

Elfu moja mia tano.

e) Eleza sifa mbili (2) za lugha ya maandishi.

i. Ni aina ya lugha ambayo huwasilishwa kwa njia ya maandishi.

ii. Ni lugha inayotumiwa na watu wanaojua kusoma na kuandika.

Kielelezo nambari 5.2 ni mfano wa mmoja wa mtahiniwa aliyejibu vizuri swali la tano. Mtahiniwa huyo anaonekana kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu vipengele vya sarufi alivyoulizwa. Katika kipengele cha 5(a) amefanikiwa kuandika mifano ya sentensi zenye makosa ya kisarufi na kimantiki. Katika kipengele (b) mtahiniwa ameweza kutoa maana mbili (2) za tungo "*Andika neno vizuri* " na "*Ali kanipigia mpira* ".

Aidha, katika kipengele cha (c) amefanikiwa kutoa mfano mmoja (1) wa mtindo wa lugha unaotumika katika mazingira ya Shuleni na Mahakamani. Katika kipengele (d) ameweza kutoa maana za misimu *Teja*, *Utajiju* na *Buku jero* na katika kipengele (e) mtahiniwa amefanikiwa kueleza sifa mbili (2) za lugha ya maandishi majibu ambayo yamemuwezesha kupata alama za juu katika swali hili.

## 3.3 SEHEMU C: FASIHI SIMULIZI

Sehemu hii ilikuwa na jumla ya maswali matatu (3) kutoka katika mada ya fasihi simulizi. Watahiniwa walitakiwa kuchagua maswali mawili (2) ambapo swali la sita (6) lilikuwa ni la lazima. Kila swali lilikuwa na jumla ya alama 15 hivyo inafanya jumla ya alama zote katika sehemu hii kuwa ni 30.

### 3.3.1 Swali la 6: Fasihi Simulizi

Swali hili lilitokana na mada ya Fasihi Simulizi katika kipengele cha Usimulizi na lilikuwa na vipengele viwili (6a) na (6b) ambapo kipengele (6a) cha swali kilimtaka mtahiniwa atoe maana ya usimulizi. Kipengele (6b) cha swali kilimtaka mtahiniwa asimulie tukio asilolisahau katika maisha yake kwa kutumia muundo wa hadithi kwa maneno yasiyozidi 120. Swali hili lilikuwa na jumla ya alama 15.

Swali hili lililenga kupima kumbukumbu ya mtahiniwa juu ya dhana ya usimulizi pamoja na uwezo wa ubunifu alionao mtahiniwa katika kusimua tukio asilolisahau katika maisha yake kwa kutumia muundo wa hadithi.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **3,927** sawa na asilimia **99.52** na **19** sawa na asilimia **0.48** hawakujibu swali la hili. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli nambari 3a.


**Jadweli nambari 3a: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 4 | | 4.5 – 9.5 | | 10 - 15 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 682 | 17.37 | 1,842 | 46.91 | 1,403 | 35.72 | 3,245 | 82.63 |

Takwimu za Jadweli nambari **3a** zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **46.91** upo katika kiwango cha wastani ambao umepelekea ufaulu wa jumla kuwa ni mzuri wa asilimia **82.63.**

Aidha, watahiniwa **682** sawa na asilimia **17.37** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na msingi mzuri kuhusu mada husika kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 6.1.

**Kielelezo 6.1 (Kibaya)**


6. a) Nini maana ya usimulizi?

Usimulizi ni nero yanayo kutumia kwa watahani kusoma Kiswahili

b) Simulia tukio usilolisahau katika maisha yako kwa kutumia muundo wa hadithi kwa maneno yasiyozidi 120.

Assalamu
Tafadhali soma hadithi hii
Kusu shoga Kuhusu Shoga
ni Shoga mpendwa
mpenzi ambayo kwa kusoma
mbali mbali katika ya
miaka Karibuni hata kwa
jeshi nchi yetu Tanzania
maisha ya kila siku ni
Kusoma
Asante

Kielelezo nambari 6.1 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa ambaye amejibu vibaya swali hili. Mtahiniwa huyu ameshindwa kabisa kutoa majibu sahihi katika vipengele vyote viwili. Majibu ya mtahiniwa yanadhihirisha wazi kuwa amekosa msingi mzuri juu ya mada ya usimulizi na hivyo kushindwa kutoa maana sahihi ya usimulizi pia ameshindwa kusimulia tukio kama swali lilivyomtaka.

Aidha, watahiniwa **1,403** sawa na asilimia **35.73** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa na ufahamu mzuri juu ya mada husika na kufahamu vyema mantiki ya maswali waliyoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 6.2

**Kielelezo 6.2 (Kizuri)**

6. a) Nini maana ya usimulizi?

Usimulizi: Ni hle hali ya kusimulia kitu kwa kutumia njia ya maandishi au mdomo

b) Simulia tukio usilolisahau katika maisha yako kwa kutumia muundo wa hadithi kwa maneno yasiyozidi 120.

Paukwa!

Pakawa!

Hapo zamani zakale palikuwepo na watu wengi sana katika kijiji cha donge. Siku mmoja watu waliku wa wanapata shida sana kwa maji hamunakila schemu. Siku zikapita nyingi Sikumoja watu wakaamuwa wajenge kisima watu walikubali lakini kuna mzee mmoja alikuwa anaitwa musa Vuai Musa alikataa kuungana na wenzake kwa kuchimba kisima watu wengine walichumbua kisima ikapita miezi Saba kisima kilipo kamilika. Saku mmoja watu walikuwa hawapo mzee musa vuai aliamuwa kunda kuyachafuwa maji alikunjwa na kuyachafua maji hapo watu wakatokea na kunadia mwizi! mwizi! mwizi mwizi tushamkamata mwizi aliyekuwa tunamtafuta kwa muda mrefu alikataa kuwenda kuchimba kusima watu wakaamua akamatwa na kupelekwa kituoni na kufungwa kwa muda wa miaka mitatu (3) jela hadi siku huyu watu wakaishi kwa furaha hiyo ni siku nisiyo isahau tena.

Kielelezo nambari 6.2 ni mfano wa mmoja wa mtahiniwa aliyejibu vizuri swali la sita. Mtahiniwa huyo anaonekana kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mada ya usimulizi. Katika kipengele cha 6(a) amefanikiwa kutoa maana sahihi ya usimulizi, pia ameweza kusimulia tukio asilolisahau katika maisha yake kwa kutumia muundo wa hadithi kwa kuzingatia idadi ya maneno yaliyotakiwa katika kipengele cha 6(b); majibu ambayo yamemuwezesha kupata alama za juu katika swali hili.

### 3.3.2 Swali la 7: Fasihi simulizi

Swali hili lilitoka katika mada ya fasihi simulizi na lilikuwa na vipengele vitano 7(a) hadi 7(e). Kipengele (a) kilimtaka mtahiniwa aeleze kwa ufupi sababu mbili (2) zinazoifanya fasihi simulizi isizeeke, kipengele (b) kilimtaka ataje vipengele vitatu (3) vya maudhui katika kazi ya Fasihi Simulizi. Kipengele (c) kilimtaka atafautishe kati ya majigambo

na vichekesho. Kipengele (d) kilimtaka aeleze sifa mbili (2) za vitendawili na katika kipengele (e) alitakiwa atoe faida mbili (2) za kazi za fasihi simulizi katika jamii. Kwa ujumla swali hili lilikuwa na alama 15.

Swali hili lililenga kupima kumbukumbu na maarifa aliyoyapata mtahiniwa katika vipengele mbalimbali vya mada ya Fasihi Simulizi.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **3,328** sawa na asilimia **84.34** na watahiniwa **618** sawa na asilimia **16.66** hawakujibu. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli nambari 3b.


**Jadweli nambari 3b: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 4 | | 4.5 – 9.5 | | 10 - 15 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 1,819 | 54.66 | 1,483 | 44.56 | 26 | 0.78 | 1,509 | 45.34 |

Takwimu za Jadweli nambari 3b zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **54.66** upo katika cha vibaya ambao umepelekea ufaulu wa jumla kuwa ni wa wastani wa asilimia **45.34.**

Aidha, watahiniwa **1,819** sawa na asilimia **54.66** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na msingi mzuri kuhusu mada husika kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 7.1.

**Kielelezo 7.1 (Kibaya)**



7. a) Eleza kwa ufupi sababu mbili (2) zinazoifanya fasihi simulizi isizeeke.
   i. Kidajwa sana
   ii. Kuandikwa

b) Taja vipengele vitatu (3) vya maudhui katika kazi ya fasihi simulizi.
   i. Vipengele
   ii. Uandishi
   iii. Matamko

c) Tafautisha kati ya majigambo na vichekesho.
   Majigambo ni kitu ambacho hupenda kujisikia
   Vichekesho ni kusema kitu cha uongo

d) Eleza sifa mbili (2) za vitendawili.
   i. Kusimulia
   ii. Kutega

e) Toa faida mbili (2) za kazi za fasihi simulizi katika jamii.
   i. Kusema
   ii. Matamshi

Kielelezo nambari 7.1 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa ambaye amejibu vibaya swali hili. Mtahiniwa huyu ameshindwa kabisa kutoa majibu sahihi katika vipengele vyote vitano alivyoulizwa. Majibu ya mtahiniwa yanaonesha wazi kuwa amekosa msingi mzuri katika vipengele mbalimbali vya mada ya Fasihi Simulizi.

Aidha, watahiniwa **26** sawa na asilimia **0.78** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa na ufahamu mzuri juu ya mada husika na kufahamu vyema mantiki ya maswali waliyoulizwa katika vipengele vyote vitano vya swali hili kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 7.2

**Kielelezo 7.2 (Kizuri)**

7. a) Eleza kwa ufupi sababu mbili (2) zinazoifanya fasihi simulizi isizeeke.

i. Fasihi simulizi haizeeki kwasababu inashirikisha fanani na hadhira.

ii. kwasababu ni mali ya jamii nzima inayorithiwa kutoka kizazi kimoja na chengine.

b) Taja vipengele vitatu (3) vya maudhui katika kazi ya fasihi simulizi.

i. Dhamira

ii. Migogoro

iii. Falsafa

c) Tafautisha kati ya majigambo na vichekesho.

Majigambo ni maigizo ya kujisifia kwa mtu kutokana na ushujaa au jambo fulani.
Vichekesho ni matumizi ya lugha kwa lengo la kuchekesha na kufikisha ujumbe fulani.

d) Eleza sifa mbili (2) za vitendawili.

i. Huwa na muundo maalumu

ii. Huwa na jibu maalumu.

e) Toa faida mbili (2) za kazi za fasihi simulizi katika jamii.

i. Zinaelimisha kwa haraka

ii. Zinaliwaza na kupunguza majonzi.

Kielelezo nambari 7.2 ni mfano wa mmoja wa mtahiniwa aliyejibu vizuri swali la saba. Mtahiniwa huyo anaonekana kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu vipengele mbalimbali vya Fasihi simulizi alivyoulizwa. Katika kipengele cha 7(a) mtahiniwa ameweza kueleza kwa ufupi sababu mbili (2) zinazoifanya fasihi simulizi isizeeke. Katika kipengele (b) amefanikiwa kutaja vipengele vitatu (3) vya maudhui katika kazi ya fasihi simulizi. Katika kipengele (c) ameweza kutafautisha kati ya majigambo na vichekesho. Katika kipengele (d) ameweza kueleza sifa mbili (2) za vitendawili na katika kipengele (e) amefanikiwa kutoa faida mbili (2) za kazi za fasihi simulizi katika jamii; majibu ambayo yamemuwezesha kupata alama za juu katika swali hili.

### 3.3.3 Swali la 8: Fasihi simulizi

Swali hili limetokana na mada ya fasihi simulizi na limegawanyika katika vipengele vitano (5) (a) hadi (e). Kipengele (a) kilimtaka mtahiniwa ataje vipengele vitatu (3) vinavyopaswa kuzingatiwa wakati wa kuigiza ngonjera. Kipengele (b) kilimtaka aeleze

maana za istilahi (i) *Sanaa za maonesho* na (ii) *Taswira*. Kipengele (c) kilimtaka atoe hoja mbili (2) kuthibitisha kauli inayosema “Fasihi simulizi ikihifadhiwa katika kanda za kunasa sauti inapoteza uhai wake.” Kipengele (d) kilimtaka ataje utanzu wa Fasihi Simulizi wenye vipera vya tarihi, ngano, vigano, soga na visasili na kipengele (e) kilimtaka mtahiniwa aeleze kwa ufupi busara za methali (i) *Mtegemea cha ndugu hufa masikini* na (ii) *Usipoziba ufa utajenga ukuta*.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima kumbukumbu na maarifa aliyoyapata mtahiniwa katika vipengele mbalimbali vya mada ya Fasihi Simulizi.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **621** sawa na asilimia **15.74** na watahiniwa **3,325** sawa na asilimia **84.26** hawakujibu swali la hili. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli nambari **3c**.

**Jadweli nambari 3c: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 4 | | 4.5 – 9.5 | | 10 - 15 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 189 | 30.43 | 283 | 45.58 | 149 | 23.99 | 432 | 69.57 |

Takwimu za Jadweli nambari 3c zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **45.58** upo katika kiwango cha wastani ambao umepelekea ufaulu wa jumla kuwa ni mzuri wa asilimia **66.57.**

Aidha, watahiniwa **189** sawa na asilimia **30.43** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na msingi mzuri kuhusu mada husika kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 8.1.

## Kielelezo 8.1 (Kibaya)

8. a) Taja vipengele vitatu (3) vinavyopaswa kuzingatiwa wakati wa kuigiza ngonjera.

i. 8 ~~Bezeni~~ Mezeni

ii. Ubeti

iii. Kipande

b) Eleza maana za istilahi zifuatazo za fasihi.

i. Sanaa za maonesho

Ni kipaji cha binadamu anaonesha katika tukio fulani.

ii. Taswira

Ni kitendo cha mwanadamu ana kuwo~~nda~~ na kilo tukio fulani

c) "Fasihi simulizi ikihifadhiwa katika kanda za kunasa sauti inapoteza uhai wake." Toa hoja mbili (2) kuthibitisha kauli hii.

i. Kuwa na ya ~~ki~~ kina na mgeni

l.

ii. Kuwa ni refu na hai na maana.

d) Tarihi, ngano, vigano, soga na visasili ni vipera vya utanzu gani wa Fasihi simulizi?

Ni vipera vya utanzu ya upaa shihuri fasihi Simulizi

e) Eleza kwa ufupi busara za methali zifuatazo.

i. Mtegemea cha ndugu hufa masikini.

Ni mtu anaongoza family ya mwenyezo.

ii. Usipoziba ufa utajenga ukuta.

Ni mtu anajifaya masikini Sana.

Kielelezo nambari 8.1 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa ambaye amejibu vibaya swali hili. Mtahiniwa huyu ameshindwa kabisa kutoa majibu sahihi katika vipengele vyote vitano alivyoulizwa. Majibu ya mtahiniwa yanaonesha wazi kuwa amekosa msingi mzuri katika vipengele mbalimbali vya mada ya Fasihi Simulizi.

Aidha, watahiniwa **149** sawa na asilimia **30.43** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa na ufahamu mzuri juu ya mada husika na kufahamu vyema mantiki ya maswali waliyoulizwa katika vipengele vyote vitano vya swali hili kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 8.2

**Kielelezo 8.2 (Kizuri)**

8. a) Taja vipengele vitatu (3) vinavyopaswa kuzingatiwa wakati wa kuigiza ngonjera.

i. Jukwaa

ii. Mavazi

iii. Wahusika

b) Eleza maana za istilahi zifuatazo za fasihi.

i. Sanaa za maonesho

Ni aina ya sanaa ambazo huganikika jukwaani au sehemu zenye mkusanyiko wa watu.

ii. Taswira

Ni muonekano wa umbo la nje la kitu au mtu.

c) "Fasihi simulizi ikihifadhiwa katika kanda za kunasa sauti inapoteza uhai wake." Toa hoja mbili (2) kuthibitisha kauli hii.

i. Huwa haiwakutanishi fanani na hadhira

ii. Hutumia gharama katika uhifadhi wake.

d) Tarihi, ngano, vigano, soga na visasili ni vipera vya utanzu gani wa Fasihi simulizi?

Ni vipera vya hadithi

e) Eleza kwa ufupi busara za methali zifuatazo.

i. Mtegemea cha ndugu hufa masikini.

Unapotaka kufanya kitu tumia nguvu zako mwenyewe na wala usitegemee kwa mtu yoyote kwani umtegemeaye huweza kukuacha mkono na ukaishia patupu.

ii. Usipoziba ufa utajenga ukuta.

Unapokiona kitu hakipo sawa au hakijakamilika unatakiwa kukikamilisha au kukifanya mapema kabla hakijaharibika chote.

Kielelezo nambari 8.2 ni mfano wa mmoja wa mtahiniwa aliyejibu vizuri swali la Nane. Mtahiniwa huyo anaonekana kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu vipengele mbalimbali vya Fasihi simulizi alivyoulizwa. Katika kipengele cha 8(a) mtahiniwa amefanikiwa kutaja vipengele vitatu (3) vinavyopaswa kuzingatiwa wakati wa kuigiza ngonjera. Katika kipengele (b) ameweza kueleza kwa usahihi maana za istilahi alizopewa. Katika kipengele (c) amefanikiwa kutoa hoja mbili (2) ili kuthibitisha kauli inayosema "Fasihi simulizi ikihifadhiwa katika kanda za kunasa sauti inapoteza uhai wake." Aidha, katika kipengele (d) mtahiniwa ameweza kutaja utanzu wa Fasihi Simulizi wenye vipera vya

tarihi, ngano, vigano, soga na visasili na katika kipengele (e) ameweza kueleza kwa ufupi busara za methali (i) *Mtegemea cha ndugu hufa masikini* na (ii) *Usipoziba ufa utajenga ukuta*; majibu ambayo yamemuwezesha kupata alama za juu katika swali hili.

### 3.4: SEHEMU D: Uandishi wa Insha na Barua

Sehemu hii ilikuwa na jumla ya maswali 2 kutoka katika mada ya Uandishi. Watahiniwa walitakiwa kuchagua swali moja tu (1) ambapo kila swali lilikuwa na jumla ya alama ishirini (20) na kufanya jumla ya alama zote katika sehemu hii kuwa ni ishirini (20).

#### 3.4.1 Swali la 9: Uandishi wa Insha

Swali hili lilitokana na mada ya uandishi katika kipengele cha uandishi wa Insha. Swali hili lilikuwa ni la kuchagua na lilikuwa na vipengele viwili ambapo mtahiniwa alitakiwa kuchagua kipengele kimoja tu kati ya kufafanua mambo matano (5) muhimu ya kuzingatia wakati wa kuandika Insha za Hoja au kuchagua kichwa cha habari kimoja kati ya *UTAMADUNI WA MZANZIBARI* na *MALEZI BORA KWA WATOTO* na kuandika Insha isiyopungua maneno 120 na yasiyozidi 150. Swali hili lilikuwa na jumla ya alama 15.

Swali hili lililenga kupima kumbukumbu na ubunifu wa mtahiniwa kuhusu utungaji wa Insha.

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA 0 – 5.5 | | WASTANI 6 – 12.5 | | VIZURI 13 - 20 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 1,165 | 43.65 | 1,009 | 37.80 | 495 | 18.55 | 1,660 | 56.35 |

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **2,669** sawa na asilimia **67.64** na watahiniwa **1,277** sawa na asilimia **32.36** hawakujibu swali la hili. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli nambari **4a**.

**Jadweli nambari 4a: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

Takwimu za Jadweli nambari **4a** zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **43.65** upo katika kiwango cha vibaya ambao umepelekea ufaulu wa jumla kuwa ni wa wastani wa asilimia **56.35.**

Aidha, watahiniwa **1,165** sawa na asilimia **43.65** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na msingi mzuri kuhusu mada ya Uandishi wa Insha kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 9.1(a) na 9.1 (b).

**Kielelezo 9.1 (a) (Kibaya)**

9. Fafanua mambo matano (5) muhimu ya kuzingatia wakati wa kuandika Insha za Hoja.

AU

Chagua kichwa cha habari kimoja kati ya vifuatavyo na uandike Insha isiyopungua maneno 120 na isiyozidi maneno 150.

- UTAMADUNI WA MZANZIBARI
- MALEZI BORA KWA WATOTO

1) Kuwepo kwa isha tafauti za hoja


2) Kuwepo kwa vipengele tofauti za hatua za kuzingatia

3) Kuwe kwa paragraf mwanza wa kutaka kuandika maswali

4) Kuwe po kwa vituo au koma katika maswali

5) Kuwepo kwa namna ya kujua jambo lipi limekusudiwa.

**Kielelezo 9.1 (b) (Kibaya)**


Ali Juma Ali
4/12/2023
ZANZIBAR

Assalamu

Tafadhali soma barua hii
Mwana Hivi karibuni nchi yetu
watu wengi ambao nchi yetu
leo siku ya malezi bora kwa watoto
familia ya nzuri mbali mbali
isipo kuwa zamani uhalifu
wakati sasa umefika serikali
na wananchi kazi makini
Afrika

Asante

Kielelezo nambari 9.1(a) na 9.1(b) ni mfano wa karatasi za watahiniwa ambao wamejibu vibaya swali hili. Katika kielelezo nambari 9.1 (a) mtahiniwa ameshindwa kutoa ufafanuzi sahihi juu ya mambo matano (5) muhimu ya kuzingatia wakati wa kuandika Insha za Hoja. Aidha, katika kielelezo nambari 9.1 (b) mtahiniwa amekwenda kinyume na matakwa ya swali kwani badala ya kuandika Insha juu ya mada alizopewa yeye alichagua moja ya mada hizo na kuandika barua ya kirafiki. Majibu ya watahiniwa hao yanadhihirisha wazi kuwa wamekosa msingi mzuri juu ya mada husika na hivyo kushindwa kutoa majibu sahihi kulingana na maswali yaliyoulizwa.

Aidha, watahiniwa **495** sawa na asilimia **18.55** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa na ufahamu mzuri juu ya mada husika na kufahamu vyema mantiki ya maswali waliyoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 9.2(a) na 9.2(b).

**Kielelezo 9.2(a) (Kizuri)**

Insha ya hoja ni aina ya Insha ambayo huandikwa kwa lengo la kutoa hoja mbalimbali.

Mambo muhimu ya kuzingatia wakati wa kuandika Insha za hoja ni:-

Kwanza; Insha za hoja lazima zifuate muundo maalumu mfano kichwa cha Insha, utangulizi, kiini na hitimisho.

Pili; Insha za hoja lazima ziandikwe kwa kuzingatia taratibu za uandishi kama vile alama na vituo.

Tatu, Insha za hoja lazima ziandikwe kwa kutumia lugha sanifu.

Nne; Insha za hoja lazima ~~zing~~ ziandikwe kwa mpangilio wa hoja.

Tano; katika Insha za hoja lazima hoja hoja zinazotolewa ziwe na mashiko.

Mambo hayo yazingatiwe wakati wa kuandika Insha za hoja.

**Kielelezo 9.2(b) (Kizuri)**

9(b)) UTAMADUNI WA MZANZIBAR.

Utamaduni wa mzanzibari ni
utaratibu ambao kila mzanzibari lazima
afuate kanuni na taratibu za kizanzibari
~~Mzanzibar~~ ku
Taratibu hizi ambazo tumezikuta tangu
mababu na mabibi zetu wakizifuata
kwa ukamilifu kabisa. Miongoni mwa
taratibu hizo ni :-
Kuvaa mavazi ya heshima : mavazi
hayo ambayo yameguswa kwa
upande wa mwanamme kazi ya kiheshima
ya kizanzibari ni kofia, suruali, viatu vya
makubazi na kadhalika. Na na kwa upande
wa wanawake ni kuvaa buibui, kanga.
Chungi na kadhalika.
Kudumisha ngoma za kiasili kama
kwa ajili ya kujibundisha mpaka Ngoma ya
kibuwa na kadhalika.
Kuheshimiana miongoni mwa watu wa kubwa
na wadogo ; watoto wadogo kuwaheshimu watu wakubwa
na kuwatumikia kama vile kuwapikea vitu
na kwa watu wazima kuwaheshimu na kuwa
heshimu watoto (wadogo).
Kuwaidiam kwa hali na mali katika jamii.
Kwahiyo tunatakiwa kulinda utamaduni
wetu na kutotukubali tamaduni za nchi nyengine.

Kielelezo nambari 9.2(a) na 9.2(b) ni mfano wa karatasi za watahiniwa ambao wamejibu vizuri swali hili. Katika kielelezo nambari 9.2 (a) mtahiniwa amefanikiwa kufafanua kwa sahihi mambo matano (5) muhimu ya kuzingatia wakati wa kuandika Insha za Hoja. Aidha, katika kielelezo nambari 9.2 (b) mtahiniwa ameweza kuandika Insha juu ya mada husika kwa kuzingatia matakwa na taratibu za uandishi wa Insha; majibu ambayo yamepelekea kupata alama za juu katika swali hili.

### 3.4.2 Swali la 10: Uandishi wa Barua

Swali hili limetokana na mada ya Uandishi katika kipengele cha Uandishi wa Barua. Swali hili lilimtaka mtahiniwa kueleza tafauti tano (5) zilizopo kati ya barua ya kirafiki na barua ya kikazi na lilikuwa na jumla ya alama 15.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima ufahamu wa mtahiniwa katika kueleza tafauti za barua ya kirafiki na barua ya kikazi.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **1,233** sawa na asilimia **31.25** na watahiniwa **2,713** sawa na asilimia **68.75** hawakujibu swali la hili. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli nambari **4b**.


**Jadweli nambari 4b: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 5.5 | | 6 – 12.5 | | 13 - 20 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 342 | 27.74 | 560 | 45.41 | 331 | 26.85 | 891 | 72.26 |

Takwimu za Jadweli nambari **4b** zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **45.41** upo katika kiwango cha wastani ambao umepelekea ufaulu wa jumla kuwa ni mzuri wa asilimia **72.26**

Aidha, watahiniwa **342** sawa na asilimia **27.74** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na msingi mzuri kuhusu mada husika kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 10.1.

**Kielelezo 10.1 (Kibaya)**


10. Eleza tafauti tano (5) zilizopo kati ya barua ya kirafiki na barua ya kikazi.

Asalamwaleikum
walekumsalam vipi hali safi kwetomo
mimi natako kuomba urafiki na wewe
jee utanikubalio

Box
CHAMBUNI
4/12/2023
ZANZIBAR Asalamwaleikum walekumsalam
vipi hali nzurita saloma wanesalimiko mimi
nimekuja nnoshida ni onekuja kuomba kazi

Kielelezo nambari 10.1 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa ambaye amejibu vibaya swali hili. Mtahiniwa huyu ameshindwa kufahamu mantiki ya swali hili na hivyo kutoa majibu yaliyokwenda kinyume na swali aliloulizwa. Mtahiniwa huyu badala ya kueleza tafauti tano (5) zilizopo kati ya barua ya kirafiki na barua ya kikazi yeye ameonesha jinsi ya kuomba urafiki na kuomba kazi; majibu ambayo hayakuwa sahihi.

Aidha, watahiniwa **331** sawa na asilimia **26.85** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa na ufahamu mzuri juu ya mada husika na kufahamu vyema mantiki ya maswali waliyoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 10.2

**Kielelezo 10.2 (Kizuri)**

10. Eleza tafauti tano (5) zilizopo kati ya barua ya kirafiki na barua ya kikazi.

Barua ya kirafiki ni barua ambayo huandikwa kwa madhumuni ya kujuliana hali au kusalimiana. Barua ya kikazi ni barua ambayo huandikwa kwa ajili ya ombi maalum. mfano wa maombi hayo ni kama ifuatavyo, kuomba ajira, kusafiri nao kuomba mapumziko kwa ajili ya kitu maalum.


Kutokana na maelezo mafupi tuliyo yapata kupitia Barua ya kirafiki na Barua ya kikazi. Hivyo zipo tofauti nyingi zinazo husu Barua ya kirafiki na Barua ya kiofisi miongoni mwa hizo tofauti ni :-

Ndaanza Barua ya kikazi huandikwa kwa maombi maalum kama vile kuomba kazi, kusafiri na n.k. Barua ya kirafiki huandikwa kwa madhumuni ya kusalimian kujuliana hali na sio kuomba kazi.

Nafuata Barua ya kikazi huwa huandikwa kwa kutumia anwani mbili ya mwandikaji na anwani ya mpokeaji. Barua ya kirafiki huandikwa kwa kutumia anwani moja nayo ni ya mwandikaji.

Pia Barua ya kikazi huandikwa kwa kumbukumbu namba. Barua ya kirafiki haiandikwi kwa kutumia kumbukumbu namba.

Kisha Barua ya kikazi huandikwa kwa kichwa cha habari mfano YAH: OMBI LA KAZI. Barua ya kirafiki haiandikwi kwa kichwa cha habari


Na Mwisho Barua ya kikazi inapo
andikwa haina salamu za majirani wala ndugu
isipokuwa kwa yule aliyo kusudiwa na kwa umoja.
Barua ya kirafiki inapoandikwa huandikwa
ndani yake salamu za majirani na hata
watu wawili au zaidi inaweza kuandikiwa
barua hiyo.
Kutokana na maelezo mengi ya
Barua ya kirafiki na Barua ya kikazi. Barua
ya kirafiki hutumika kwa salamu za ndugu
na jamaa nyumbani na Barua ya kikazi
hutumika kwa maombi ya ajira na n.k

Kielelezo nambari 10.2 ni mfano wa mmoja wa mtahiniwa aliyejibu vizuri swali la Kumi. Mtahiniwa huyo anaonekana kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mada ya Uandishi wa Barua na hivyo amefanikiwa kueleza kwa usahihi tafauti tano (5) zilizopo kati ya barua ya kirafiki na barua ya kikazi; majibu ambayo yamemuwezesha kupata alama za juu katika swali hili.

## 4.0 HITIMISHO

Uchambuzi wa maswali katika somo la Kiswahili unaonesha kwamba watahiniwa walifanya vizuri na kupata alama za juu katika maswali sita (6) kati ya hayo ni swali nambari 1 linalotokana na mada ya Ufahamu ambalo lilipata asilimia 90.13 ya ufaulu, swali nambari 2 linalotokana na mada ya Ufupisho wa habari ambalo lilipata asilimia 82.94 za ufaulu, swali nambari 5 linalotokana na mada Matumizi ya lugha ambalo lilipata asilimia 80.28 ya ufaulu, swali nambari 6 linalotokana na mada ya Fasihi Simulizi ambalo lilipata asilimia 82.63 ya ufaulu, swali nambari 8 linalotokana na mada ya Fasihi Simulizi ambalo lilipata asilimia 69.57 ya ufaulu na swali nambari 10 linalotokana na mada ya uandishi wa Barua ambalo lilipata asilimia 72.26 ya ufaulu.

Pia uchambuzi unaonesha kuwa jumla ya maswali matatu (3) yalipata alama za wastani, maswali hayo ni pamoja na swali nambari tatu (3) linalotokana na mada ya vipengele vya sarufi ambalo lilipata asilimia 30.68 ya ufaulu, swali nambari saba (7) linalotokana na mada ya fasihi simulizi ambalo lilipata asilimia 45.34 ya ufaulu na swali nambari tisa (9) linalotokana na mada ya Uandishi wa Insha ambalo lilipata asilimia 56.35 ya ufaulu.

Uchambuzi huu unaonesha kwamba swali moja (1) tu ndilo lililopata ufaulu mbaya ambayo ni swali nambari nne (4) linalotokana na mada ya vipengele vya sarufi ambalo limepata asilimia 6.79 ya ufaulu.

Kwa upande mwengine uchambuzi huu unaonesha changamoto mbalimbali ambazo hazina budi kutatuliwa. Changamoto hizo ni pamoja na watahiniwa kushindwa kufahamu maelekezo ya maswali husika, uelewa mdogo wa mada mbalimbali pamoja na kuwa na uwezo mdogo wa kukumbuka kile walichojifunza darasani pamoja na kutokujua kuandika.

Mwisho taarifa hii kuhusu ufaulu wa watahiniwa itasaidia kuinua kiwango cha ufaulu katika somo la Kiswahili na kutoa msaada kwa walimu na wanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji wa mada mbalimbali pamoja na kujenga uelewa mzuri utakaowezesha kufanya marekebisho ambayo yatasaidia katika kuongeza kiwango cha ufaulu katika mitihani ijayo.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Kutokana na tathmini iliyofanywa changamoto mbalimbali zimebainika kama zilivyoainishwa katika kifungu 4.0. Ili kuzikabili changamoto hizo pamoja na kuinua kiwango cha ufaulu wa somo la Kiswahili mambo yafuatayo hayana budi kuzingatiwa.

a) Walimu waweke mkazo katika mada za vipengele vya sarufi.

b) Walimu wawahamasishe wanafunzi kuzitumia maktaba kwa ajili ya kusoma vitabu na kamusi za lugha mbalimbali ili waongeze ufanisi katika kujifunza.

c) Wanafunzi ni vyema wapatiwe mazoezi na majaribio ya mara kwa mara hasa katika utungaji, vipengele vya sarufi na fasihi kwa ujumla ili waweze kufahamu mahitaji ya swali na kuweza kufanya mitithani yao vizuri na kwa usahihi.

d) Walimu wahamasishwe kutumia mbinu shirikishi wakati wa ufundishaji hasa katika mada za viengele vya sarufi pamoja na fasihi simulizi.

e) Walimu wanashauriwa kutumia Kiswahili sanifu wakati wa ufundishaji na kuwasisitiza wanafunzi kutumia lugha sanifu katika mitihani yao ili kuepuka wanafunzi kujibu mitihani yao kwa kutumia lahaja.

f) Walimu wawape wanafunzi kazi za kutosha za darasani na nyumbani hasa zinazohusiana na masuala ya Sarufi, Fasihi Simulizi na uandishi. Hii itasaidia kuwafanya wanafunzi kuwa wabunifu, kuwa na kumbukumbu nzuri, kuwa na uandishi mzuri, kuwajengea uwezo wa kujieleza na hata kuwaweka tayari kwa ajili ya mitihani ya Taifa.

## VIAMBATANISHO

### KIAMBATANISHO NAMBARI 1

UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA SWALI NA MADA KATIKA SOMO LA KISWAHILI MWAKA 2023

| NA. | MADA | NAMBA YA SWALI | ASILIMIA YA UFAULU | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Ufahamu | 1 | 90.13 | VIZURI |
| 2 | Ufupisho | 2 | 82.94 | VIZURI |
| 3 | Fasihi Simulizi | 6 | 82.63 | VIZURI |
| 4 | Matumizi ya Lugha | 5 | 80.28 | WASTANI |
| 5 | Uandishi | 10 | 72.26 | WASTANI |
| 6 | Fasihi Simulizi | 8 | 69.57 | WASTANI |
| 7 | Uandishi | 9 | 56.35 | WASTANI |
| 8 | Fasihi Simulizi | 7 | 45.34 | WASTANI |
| 9 | Sarufi | 3 | 30.68 | VIBAYA |
| 10 | Sarufi | 4 | 6.79 | VIBAYA |